

Ardhi/maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za uwezesaji wananchi kiuchumi

Maeneo haya yana huduma muhimu na miundombinu iliyo bora. Aidha, kuwepo na uthibitisho kuwa maeneo hayo yanatumiwa na jamii/wananchi

Halmashauri ya Mji Geita imetenga maeneo kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali kwa makundi ya vijana na wanawake ili kukuza uchumi/uwezesaji wananchi kiuchumi, Halmashauri imetenga masoko matatu kwa ajili ya kutoa fursa za biashara ndogondogo kwa wanawake na vijana wajasiriamali ili kuweza kuzitumia kwa ajili ya shughuli zao za uzalishaji mali, masoko hayo yaliyotengwa ni Soko la mitumba msufini, Soko la katundu na Soko la jioni la nyankumbu, maeneo hayo yamewekewa huduma muhimu na miundombinu kama barabara, vyoo, umeme na maji.

Halmashauri ya mji kupitia idara ya ardhi na mipango miji kwa imetenga zaidi ya eneo la ekari 689 (ekari 103 Mpomvu na 586 eneo la ibanda) kwajili ya uwekezaji wa viwanda vya kati na vikubwa uwezesaji wananchi kiuchumi kama ifuatavyo:-

- **Eneo la viwanda vidogo vidogo (sido) na vya kati,**
eneo la viwanda vidogo vidogo limetengwa Mpomvu katika Kata ya Mtakuja. eneo hilo lina ukubwa wa ekari 103 na lipo kushoto mwa barabara iendayo katoro kutokea Geita mjini. Uwekezaji mkubwa wa machinjio ya kisasa yanayofadhiliwa na Benki ya Dunia unatekelezwa katika eneo hili na ujenzi wake unaendelea.
- **Eneo la viwanda vikubwa na vya kati**
Halmashauri ya Mji imetenga eneo lenye ekari 586 Mtaa wa Ibanda Kata ya Kanyala.
- **Soko la mitumba msufini**
Soko la mitumba la msufini lina ukubwa wa mita za mraba 5570 sawa na ekari 1.37 lipo Mtaa wa msufini Kata ya Kalangalala. Soko hili kwa sasa linatumika na wafanya biashara wadogo wadogo.
- **Soko la katundu**
Soko la katundu lina ukubwa wa mita za mraba 14,000 sawa na ekari 3.45 lipo mtaa wa katundu. Soko hili kwa sasa linatumika na wafanyabiashara wadogo wadogo.

- **Soko la nyankumbu**

Soko la jioni la Nyankumbu lipo upande wa kushoto mwa barabara kuu itokayo Geita mjini kuelekea Katoro mbele ya soko kuu la Nyankumbu. Soko hili limetengwa maalumu kwa ajili ya vijana wajasiriamali.

Pia kuna idadi ya wawekezaji waliovutiwa na kuwekeza katika Halmashauri ya Mji Geita

Halmashauri ya Mji Geita imetenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji na shughuli za uzalishaji mali ili kukuza uchumi na kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji kuja kuwekeza viwanda vinavyojishughulisha na shughuli mbalimbali kama uchenjuaji wa madini ya dhahabu na kopa, viwanda vya kuchambua pamba eneo la Kanyala, viwanda vya kusaga na kukoboa nafaka (mchele na mahindi), viwanda vya kutengeneza mikate.